



BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)



1. MFUMO WA USIMAMIZI WA MIRADI (PMS) SAJILI MTANDAONI ni nini?

Ni Tathmini ya Athari za Mazingira na mfumo wa usimamizi wa ukaguzi Mazingira

Baraza linasimamia miradi inayofanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa njia ya kielektroniki kupitia usajili wa mitandaoni (<http://eia.nemc.or.tz>) njia hii inamuwezesha mwekezaji kuanzisha mchakato wa Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) au Ukaguzi wa Mazingira (EA) kupitia mfumo wa usimamizi wa miradi (PMS)

i) Malengo ya Usajili wa Mtandaoni

- Kuungeza ufanisi katika mchakato wa TAM/Ukaguzi wa mazingira kwa kuokoa gharama na wakati kwa pande zote zinazohusika
- Unamwezesha mwekezaji kufuatilia kwa urahisi maendeleo ya mradi
- Unawezesha upatikanaji na utunzaji wa taarifa za TAM sehemu moja

ii) Zifuatazo ni hatua zinazopaswa kufuatwa wakati wa usajili wa miradi kwa njia ya mitandao

Hatua ya kwanza ni: Usajili (Registration): Mwekezaji hujaza fomu ya usajili kwa njia ya mtandao na kulipa ada ya usajili kwa muhtasari wa mradi.

Hatua ya pili ni: Uchunguzi wa kina (Scoping): Mwekezaji kwa kushirikiana na Mtaalamu elekezi atawasilisha Mawanda ya mradi (Scoping report) pamoja na Hadidu za Rejea (ToR) zitakazooonesha jinsi tathmini hiyo itakavyofanyika.

Hatua ya tatu ni: Tathmini ya Athari kwa mazingira: Mwekezaji atalipia gharama ya kupitia mradi na kuingiza ripoti ya TAM/Ukaguzi wa mazingira kupitia PMS

Hatua ya nne ni: Mapitio ya taarifa za mradi (Review): Baraza litatembelea eneo la mradi husika, kuwasiliana na wadau wa mradi na kupata maoni yao. Hii hufuatiwa na kikao cha kamati ya ushauri (Technical Advisory Committee meeting)

Hatua ya tano ni: Mapendekezo ya Kamati ya ushauri (Recommendations of the Technical advisory Committee TAC): Mshauri elekezi atawasilisha andiko lililoboreshwa kwa Baraza likijumuisha maboresho yaliyopendekezwa na wadau na kamati na kisha kuingizwa kwenye mfumo

Hatua ya sita ni: Kuwasilisha mapendekezo kwa Mh. Waziri (Submission to the Minister of Environment): Baraza litawasilisha mapendekezo ya mradi kwa Mh. Waziri mwenyi dhamana ya Mazingira kwa hatua zaidi

Hatua ya saba ni: Kuidhinishwa kwa ripoti ya TAM/Ukaguzi wa mazingira (Approval of the EIS/EA): Baada ya kusainiwa kwa Cheti na Waziri, kitarejeshwa NEMC kwa ajili ya kukabidhiwa mwekezaji. Waziri anaweza kuidhinisha au kutoidhinisha TAM/Ukaguzi wa Mazingira ndani ya siku 30 kulingana na Sehemu ya 92(1) ya EMA Cap. 191

Hatua ya nane ni: Kuidhinishwa kwa mradi (Issuance of Certificate): Waziri ataidhinisha uendelezaji wa mradi kwa kusaini cheti na kukabidhi kwa mwekezaji.

2. Usajili wa Mtandaoni kwa makampuni ya Wataalamu Elekezi na Mtu Binafsi

Hii itawezesha Wataalamu wa Mazingira kuingia kwenye mfumo na kuona/kufanya kazi miradi wanayopewa kutumia hati zao za kuingia badala ya ile ya wawekezaji. Ruhusa haitahusisha kufuta/kusashira taarifa lakini badala yake mfumo utaruhusu wataalam: -

- Kuangalia miradi iliyosainiwa kwao
 - Kukagua nyaraka baada ya kuidhinishwa na mwekezaji
- ### i) Malengo ya usajili wa mtaalamu wa mazingira mtandaoni
- Kuungeza ufanisi
 - Kupata taarifa sahihi kutoka kwa wataalamu wa mazingira
 - Kuboresha utunzaji kumbukumbu

- Kuwezesha utengano wa majukumu kati ya mshauri elekezi na mwekezaji
- Kuboresha ukusanyaji wa ada

ii) Hatua za kufuata kwenye usajili wa wataalamu elekezi wa mazingira kwa kampuni/mtu binafsi

Hatua ya kwanza ni: Ingia kwenye mfumo wa kielektroniki wa usajili wa mitandaoni (<http://eia.nemc.or.tz>)

Hatua ya pili ni: Fungua sehemu ya Wataalamu wa Mazingira (Experts)

- Ikiwa mtaalamu elekezi tayari ana akaunti attingia moja kwa moja
- Ikiwa mtumiaji ni mara ya kwanza atapaswa kujisajili kwa kujaza fomu ya mtandaoni na baada ya kujisajili ujumbe utatumwa kwenye akaunti yake ya barua pepe

Hatua ya tatu ni: Kamilisha akaunti yako kwa kubofya kiunga kilichotumwa kwenye barua pepe yako.

Hatua ya nne ni: Jaza maelezo binafsi

Hatua ya tano ni: Usajili au uainishaji wa mtu binafsi na kampuni ya wataalamu

Hatua ya sita ni: Kuweka/kujaza maelezo na kuweka nyaraka kulingana na Kanuni za wataalamu za 2021

NB. Kwa makampuni: anaetengeneza akaunti anapaswa kualika kiongozi mwenza (lead expert) kwa kuongoza ambao watapata taarifa ya kuomba ubia

Hatua ya saba ni: Baada ya kukamilika kwa malipo ya ada husika, maombi yanaweza kuwasilishwa kwa maamuzi

iii) Matarajio

- Kupunguza malalamiko kutoka kwa mwekezaji kwenda kwa mtaalamu elekezi
- Kupunguza mzigo wa kazi kwa wafanyakazi wa NEMC
- Kuboresha uwajibikaji
- Kuungeza uwazi

Mambo ya kuzingatia:

- Kwa mujibu wa kifungu cha 82 na 230 cha Sheria (Sura 191) kikisomwa kwa pamoja na kanuni ya (14A ya GN.No.474/2018) pindi mradi utakapokuwa umesajiliwa na hakuna hatua zozote zitakazoendelea kwa upande wa mwekezaji kwa kipindi cha miaka miwili, mradi huo utaondolewa kwenye usajili na mhusika atatakiwa kusajili upya.
- Usajili wa wataalamu elekezi wa mazingira mtandaoni utafanyika kwa kuzingatia kanuni ya 18 na 19 ya 2021.
- Ikiwa unahitaji msada wa kiufundi au maelezo zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe: eiasupport@nemce.or.tz



Mkurugenzi Mkuu
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi
wa Mazingira (NEMC)

Kambarage Tower, 6th Floor

P.O Box 2724, Dodoma, Tanzania,

Tel: +255 26 2960 098, +255 713 608 930,

Nukushi: +255 22 277 4901, WhatsApp: +255 737 796 252

Email: dg@nemc.or.tz | Website: www.nemc.or.tz

@nemctanzania

Namba ya dharura: 0800110116

www.nemc.or.tz

NEMCTV Tanzania

#MazingiraYetuUhaiWetu



NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL (NEMC)



PROJECTS MANAGEMENT SYSTEM (PMS)

What is PMS.

PMS is an online ICT based system at the NEMC . Through PMS, NEMC now manages environmental assessments electronically. The system enables registration and management of environmental assessments (EIA and EA) as well as registration and management of environmental experts. The address (URL) of the system is <https://eia.nemc.or.tz>

Objectives of PMS includes to:

- Increase efficiency in the EIA/EA processes by saving cost and time to all involved parties;
- Enable the developer/proponent to easily monitor the project progress;
- Centralize and archive EIA/EA data/information.

A: Registration and management of EIA and EA:

Steps to be followed during registration of projects online:-

Step 1: Registration: The developer fills the online registration form, uploads the project brief and pays the registration fee.

Step 2: Scoping: Developer together with the Environmental Expert prepare a Scoping Report and Terms of References (TORs) for conducting the Environmental Assessment, (EIA or EA).

Step 3: Environmental study: The developer pays charges for review and uploads EIA/EA document.

Step 4: Review: NEMC arranges for site verification by a Cross- sectoral Technical Advisory Committee (TAC).

Step 5: Recommendations of the Technical Advisory Committee (TAC): The developer will make improvements of the EIA/EA report by incorporating all comments and recommendations raised by the TAC and upload the response and an improved report to the PMS.

Step 6: Submission of report and recommendations to the Minister for Environment: The developer will upload the improved version of the EIA/EA report and if satisfactory, NEMC will forward recommendations to the Minister for Environment for final approval

Step 7: Approval /disapproval of the EIA/EA report: Upon signing of the Certificate by the Minister, it will be brought back to NEMC for collection by the developer. The Minister may approve or disapprove of the EIS/EA within 30 days as per Section 92(1) of EMA Cap. 191.

Step 8: Issuance of Certificate: The signed EIA/EA Certificate will be handed over to the developer together with the General and Specific conditions that must be adhered to by the developer during lifetime of the project.

B: Registration and management of environmental experts.

This system allows environmental experts to register then log in to the system for viewing/working on projects they are contracted to do by developers. The system does not allow to delete or update information but rather the system will allow experts to:-

- i. View projects contracted to them
- ii. Upload documents upon approval by the developer/proponent

Objectives of the Online Environmental Expert Registration include:

- Improved efficiency
- Correct information from the environmental experts
- Improved record keeping
- Separation of roles between consultant and developer
- Enhance fee collection

Steps to follow for Registration of Environmental Experts Firm/Individual

Step 1: Access the system through the link <https://eia.nemc.or.tz>.

Step 2: Click on the menu Experts

- If Existing Expert, click sign in
- If is a first time user, click sign up. After signing up, a message will be sent to your email account for activation

Step 3: Activate your account by clicking the link sent to your email

Step 5: Fill in your personal details

Step 6: Choose action, whether is Registration of individual or a Firm of Experts

Step 7: Create an account by filling details and upload documents as required by Experts Regulations of 2021

Note. For Firms, the creator of the account has to invite lead experts who will receive notification requesting for partnership.

Step 8: Upon completion and payment of relevant fee, the application can be submitted to NEMC online for review

Expectations:

- Reduce complaints from the developer/proponent to the environmental expert
- Reduce workload to NEMC staff
- Improved accountability



Director General,
National Environment Management
Council (NEMC)

Kambarage Tower, 6th floor
S.L.P 2724, Dodoma Tanzania

Tel: +255 26 2960098, +255 713 608 930

Fax: +255 22 2774901

WhatsApp: +255 737 796 252

Web: www.nemc.or.tz

Email: dg@nemc.or.tz



Toll free: 0800110116

www.nemc.or.tz

NEMCTVTanzania

#OurEnvironmentOurLife#